MUHTASARI WA KISERA

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

# Katika Kutafuta Usimamizi wa Pamoja wa Misitu Tanzania….

Wakati Tanzania imepata sifa sana kwa kujumuisha Usimamizi wa pamoja wa Misitu katika sera, kwa muda mrefu jamii imekuwa ikilaumu kwamba Serikali bado haijaweka dhamira ya kweli kutekeleza makubaliano yaliyopo katika sera. Mikataba ya usimamizi shirikishi imebaki bila kusainiwa kwa muda mrefu, kugawana faida hakuja tekelezwa wakati jamii maskini wanaendelea kuchukua majukumu ya ziada katika kusimamia misitu. Katika utafiti ndogo uliohusisha vjiji 15 vinavyoshiriki katika usimamizi wa pamoja wa misitu, tuligundua kuwa usimamizi wa pamoja wa misitu uko katika hali ya nadharia zaidi kuliko hali halisi. Tunauomba wakala wa misitu Tanzania ulioanzishwa mwaka huu kufikiri tena juu ya mfumo wa Usimamizi wa pamoja wa misitu.

**Usimamizi wa Pamoja wa Misitu** = Jamii zinashirikiana na serikali kuu au serikali za mitaa katika kusimamia misitu ya serikali kuu au serikali za mitaa.

**Misitu inayosimamiwa na jamii pekee** = Jamii kusimamia misitu iliyopo katika ardhi ya kijiji au ardhi katika maeneo ya jamii au hifadhi za misitu za vijiji.

Kijarida hiki kinalenga Usimamizi shirikishi wa misitu. Hali katika misitu inayosimamiwa na jamii pekee imekuwa ya kuridhisha katika masuala ya usimamizi na kugawana faida.

## Usimamizi wa Pamoja wa Misitu: Umedhamiriwa vizuri ila haujatekelezwa vizuri

Tanzania ilianzisha usimamizi wa pamoja wa misitu katika Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 *'ili kuboresha uhifadhi na usimamizi wa misitu na kuhakikisha mgawanyo sawa wa manufaa miongoni mwa wadau wote ikiwa ni pamoja na jamii za vijijini.'* Kwa kutambua kwamba Serikali peke yake haiwezi kuzuia uharibifu katika misitu ya hifadhi na kwa kutambua kuwa kuna haja ya kuwa na namna ya ushirikiano na usawa wa mgawanyo wa faida, ndipo sera ikapitishwa. Hapo ilifuatia miaka takribani 13 ya majaribio na kusisitiza usimamizi shirikishi wa misitu huku washirika wa maendeleo wakiwekeza mamilioni ya dola katika mchakato huo.

Mwaka 2008 Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT) ilitoa ripoti "Sensa ya Taifa ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu" ikionyesha hali ya Usimamizi wa Pamoja wa Misitu. Kulingana na takwimu zilizotolewa kutoka wilaya 85 ambazo zinatekeleza usimamizi shirikishi wa misitu, sensa ilionyesha kuwa hekari milioni 1.6 za misitu katika hifadhi za misitu 209 zilikuwa chini ya usimamizi wa pamoja na vijiji. Tafiti mbalimbali ambazo zilichapishwa takribani kwa wakati mmoja zilionyesha kuwa misitu inayosimamiwa kwa ushirikiano kati ya serikali na vijiji ipo katika hali nzuri zaidi kuliko misitu ambayo inasimamiwa na serikali pekee. Maana mojawapo ya matokeo haya ya tafiti inaweza kuelezwa kuwa ni matokeo ya kupatikanika kwa faida ambayo imekuwa kama motisha isio rasmi kwa jamii na hivyo jamii kuendelea kushiriki katika usimamizi wa misitu. Hata hivyo, kwa zaidi ya miaka kadhaa, TFCG na MJUMITA zimeendelea kupata malalamiko kutoka kwa jamii kutoka kote nchini kuwa Serikali bado haijatimiza majukumu yake kuhusu usimamizi wa pamoja wa misitu. Jamii zinalalamika serikali kushindwa kurudisha mikataba iliyosainiwa kwao, na hivyo kutopata sehemu ya mapato na kushindwa kutekeleza mipango ya usimamizi.




*Mgawanyo wa faida na gharma katikia usimamizi wa pamoja wa misitu*

## Je, takwimu za sensa ya usimamizi shirikishi wa misitu zinashabiana na uzoefu wa jamii kwenye usimamizi wa pamoja wa misitu?

Ili kujua zaidi ni uzoefu gani jamii imepata katika kushiriki katika usimamizi wa pamoja wa misitu, tuliuliza Serikali za vijiji na / au kamati za maliasili katika vijiji 15 kutoka kanda tatu za kitaifa, ambavyo vilitajwa katika Sensa ya Taifa ya usimamizi shirikishi wa misitu kuwa vinashiriki katika usimamizi wa pamoja wa misitu, kuhusu uzoefu wao. Maswali na majibu yalikuwa kama ifuatavyo:-

Je, kijiji chako kimetengeneza na kuidhinisha mpango wa usimamizi wa misitu, sheria ndogo na mkataba wa usimamizi wa pamoja wa misitu?
Vijiji 15 vikasema ndiyo. Kwa wastani waliidhinisha mipango ya usimamizi wa misitu miaka 7 iliyopita na kuwasilisha kwa Idara ya Misitu na Nyuki.

Je, Idara ya Misitu na Nyuki imesaini na kurudisha mkataba wa usimamizi wa pamoja wa msitu kwa kijiji chako? kijiji kimoja kilisema ndio. Vijiji 14 vilisema hapana.

Je, serikali imerudisha mapato yoyote kwenu kama ilivyoainishwa katika makubaliano ya usimamizi wa pamoja wa misitu? Vijiji 15 vilisema hapana

Je, jamii yako bado ina nia ya kushiriki katika usimamizi wa pamoja wa misitu? Vijiji 14 vilisema ndiyo, kijiji kimoja kilisema hapana

Vijiji vilieleza kuwa bado wanategemea misitu ili kupunguza mmomonyoko wa udongo; kupata maji wakati wa kiangazi na mazao ya misitu yasiyotokana na mbao. Jamii walionyesha nia ya kushirikiana na serikali lakini vijiji vyote 15 vilieleza hali ya misitu ya hifadhi imeendelea kuwa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita wakati masuala ya usimamizi wa pamoja yakiwa yanajadiliwa. Vijiji vimeitaka serikali kuchukua hatua za haraka ili kuokoa misitu iliyobaki.

*Ni nini kinatakiwa kufanywa ili usimamizi wa pamoja wa misitu ufanye kazi vizuri?*
Ili usimamizi wa pamoja wa misitu ufanye kazi vizuri, Wanavijiji waliohojiwa, waliomba serikali:

- kutekeleza ahadi zake ikiwa ni pamoja na kutia saini makubaliano.
- kutoa sehemu ya mapato kwa jamii.
- usambazaji wa vifaa kwa ajili ya doria na usafishaji wa mipaka ya misitu.
- Kuwalipa wale ambao wanashiriki katika doria na kazi nyingine za usimamizi wa misitu.

## Nini kinazuia Idara ya Misitu na Nyuki kusaini mikataba?

Ilipoulizwa kuhusu sababu ya kuchelewa kusaini mikataba, Idara ya Misitu na Nyuki ilisema kwamba Wizara ya Fedha imekataa kuruhusu fedha za serikali kukusanywa na kusambazwa kwa njia ambayo ilikubaliwa wakati mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu ulipokuwa unaanzishwa. Kwa uanzishwaji wa hivi karibuni wa wakala wa misitu Tanzania, kikwazo hiki kimeondolewa.

## Je, ni nini kinachohitajika ili usimamizi wa pamoja wa misitu ufufuke?
## Kutambua kuwa Usimamizi wa pamoja wa misitu unaweza kufanya kazi vizuri ila juhudi zinatakiwa kufanyika.

Wakati sera ya Taifa ya Misitu ikionyesha nia ya usimamizi wa pamoja wa misitu ili kuboresha usimamizi na kuwa na usawa zaidi, kumekuwa na matumaini yasiyozungumzwa kwamba hii pia itakuwa njia nafuu ya kufidia upungufu wa bajeti katika sekta ya misitu. Katika miaka kumi iliyopita, washirika wa maendeleo wamekuwa wakisaidia kupunguza ufinyu huu wa bajeti lakini kama usimamizi wa misitu wa pamoja unatakiwa kuwa ndio sera kuu katika sera ya taifa ya misitu, kuna haja ya kuwa na dhamira ya kweli na utashi wa kisiasa wa kulipa gharama halisi ya usimamizi wa pamoja wa misitu kwa jamii. Wanakijiji wanaoshughulika na usimamizi wa misitu wanatakiwa kulipwa kwa kazi wanayofanya. Doria misituni, kutengeneza mipaka ya misitu na shughuli za kuzuia moto misituni ni kazi ngumu. Sio sawa kwa baadhi ya jamii ambazo ni masikini kufanya kazi za kulinda mifumo ya huduma za kiikolojia ambazo zinanufaisha taifa zima bure bila malipo. Kwa maana hiyo jamii zinazoishi kando kando mwa misitu haipaswi kuonekana kama chanzo cha nguvu kazi ya bure ya kufanya kazi ngumu kwenye usimamizi wa misitu. Kama hali hii ikiendelea ni dhahiri kuwa usimamizi wa pamoja wa misitu hautafikia malengo ya sera yaliyokusudiwa na kuna uwezekano wa mgawanyiko kati ya jamii na mamlaka za usimamizi wa misitu kuongeza.

## Wakala wa misitu Tanzania wanatakiwa kutekeleza ahadi zilizowekwa katika makubaliano ya usimamizi wa pamoja wa misitu.

Baada ya uzinduzi wa wakala wa misitu Tanzania na mfuko wa misitu Tanzania, ni wakati muafaka sasa wa kurejea, kupitia upya na kusaini makubaliano ya usimamizi wa pamoja wa misitu na kutekeleza ahadi zilizowekwa kwenye sera ya misitu za kuhakikisha misitu ya taifa inahifadhiwa kwa njia endelevu.

Kijarida hiki kimetengenezwa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa kushirikiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kupitia mradi wake wa "Haki katika Misitu".

Kwa mawasiliano zaidi, andika barua kwa:
Mkurugenzi Mkuu, TFCG,
S.L.P 23410, Dar es Salaam na/au
Mkurugenzi Mkuu, MJUMITA,
S.L.P 21522, Dar es Salaam`
http://www.tfcg.org/forestJusticeTanzania.html